# Pwani Leo

*Kazi iendelee...*

Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani

12 Mei 2022 | www.Pwani.go.tz | Toleo Maalum la Mwenge wa Uhuru

## Pwani yavuka lengo uandaaji anuani za makazi.Uk...2

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa



Pichani ni Mkuu wa Mkoa wa Lindi Mhe. Zainab Telak Akimkabidhi Mwenge wa Uhuru Mhe.Abubakari KunengeMkuu wa Mkoa wa Pwani Kijiji cha Kiwanga Wilayani Rufiji.

# PwaniLeo
Toleo Maalum la Mwenge wa Uhuru Kazi iendelee...

Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani


## Pwani yavuka lengo uandaaji anuani za makazi.

**Rufiji Pwani**
**Na.Nasra Mondwe**

Jumla ya nyumba 515,668 zimeingizwa kwenye mfumo wa Zoezi la anwani za makazi sawa na asilimia 105.61 Mkoani Pwani.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani Abubakar Kunenge alipotoa taarifa ya Mkoa Kwa kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru za Mwaka 2022.

Katika mapokezi ya Mbio za Mwenge wa Uhuru za Mwaka 2022 ambayo yamefanyika katika Kijiji cha Kiwanga Wilayani Rufiji kutoka Mkoa wa Lindi leo Mei 1, 2022, Mkuu wa mkoa wa Pwani Abubakari Kunenge alisema kufuatia maandalizi ya sensa na makazi Mkoa wa Pwani umejipanga na kuendelea kuhimiza wananchi kujitokeza kwenye Zoezi hilo litakalotekelezwa mwezi Agost mwaka huu.

"Mkoa wetu ni miongoni mwa mikoa 13 iliyoshiriki kwenye zoezi la sensa ya majaribio na Tunashukuru tumefanya vizuri " Kunenge alisema.

Mkuu huyo wa mkoa alieleza kuwa,kiasi cha sh.milioni 816 .2 kutoka Serikali Kuu kimepokelewa na Halmashauri zimechangia milioni 320.

Pamoja na hayo, Kunenge alieleza mwenge wa uhuru ukiwa Mkoani hapo utapitia miradi 111 yenye gharama ya Zaidi ya Bilioni 69.2.

"Kati ya miradi hiyo miradi 25 itawekwa mawe ya msingi, 22 itazinduliwa,6 itafunguliwa na 58 kukaguliwa"alifafanua Kunenge.

Akipokea mwenge wa uhuru Mkuu wa wilaya ya Rufiji Edward Gowelle kutoka kwa Mkuu wa mkoa,alisema mwenge ukiwa Rufiji utapitia miradi sita yenye thamani ya milioni 600.5.

Kati ya miradi iliyotembelewa Rufiji ni pamoja na Zahanati Nyanda Katundu, barabara Mji Utete, mradi wa vijana kikundi cha Kumekucha Umwe Kaskazini, Mradi wa Uraghibishaji falsafa ya mwenge,ghala la mwananchi na madarasa ya Sekondari Mkongo. Mwenge wa uhuru Mei 2 unatarajiwa kupokelewa huko Mkupuka wilaya ya Kibiti.



# PwaniLeo

Toleo Maalum la Mwenge wa Uhuru *Kazi iendelee...*

**Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani**


## Matukio mbalimbali ya Mapokezi ya Mbio za mwenge Wilayani Rufiji Mkoa wa Pwani




























# Geraruma ahimiza uhifadhi miradi ya Maji

**Kibiti Pwani,**
**Na.Nasra Mondwe**

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Sahil Geraruma, ameiasa jamii kulinda na kuhifadhi tanki la Kisima na kujiepusha na jambo lolote linaloweza kuleta madhara kwa watumiaji.

Akizindua mradi wa tanki la maji katika Zahanati ya 830 KJ Kibiti Mkoani Pwani ambao umekamilka kwa asilimia 100 na ulio tayari kutoa huduma ndani ya jamii inayoizunguka, Geraruma amepongeza usimamizi mzuri katika kutekeleza mradi huo.

Awali akisoma taarifa ya mradi, Kapt. Yusuph Matias Masalu wa 830 KJ Kibiti alisema kikosi kilianza jengo la muda la Zahanati Lakini baadae makao makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa kutumia fedha za maendeleo ya mwaka wa fedha 2020-2021.

“Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kupitia ufadhili wa Shirika la “global A Network” linalotoa msaada wa kuchimba visima virefu Kibiti kwa kushirikiana na Wakala wa maji safi na usafi wa Mazingira Vijijini ( RUWASA) wameweza kutekeleza mradi huo pamoja na visima vingine 19 vyenye thamani ya sh. milioni 380 wilayani hapa”. Alisema Kapt. Masalu.

Kuhusu thamani ya ujenzi wa mradi huo, Masalu alibainisha kuwa wafadhili hao na RUWASA walifanya utafiti wa maji chini ya ardhi na kuchimba kisima hicho ,chenye uwezo wa kuzalisha maji lita 11,300 kwa saa na urefu wa mita 93 kilichogharimu milioni 20 .

Alieleza, kikosi hicho kimetumia milioni 15.1 Kwa Ajili ya kupima wingi, ubora wa maji, kujenga mnara, kununua tanki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita 10,000, kununua na kufunga pampu kwa Lengo la kutoa huduma ya maji.

Mkuu wa wilaya ya Kibiti, kanal Ahmed Abbas alisema mwenge wa Uhuru ukiwa wilayani humo utapitia miradi 15 yenye thamani ya sh.milioni 809.3 na kukimbizwa km.110 kwenye kata tano.

Miradi mingine iliyopitiwa ni Pamoja na ujenzi wa vivuko vitatu kwenye bonde la Nyarwanza, ujenzi wa madarasa matatu kwa fedha za Uviko 19, mradi wa madarasa matatu katika Shule ya Sekondari Mtawanya kwa fedha za mapato ya ndanimradi wa kituo cha afya Mjawa na shamba la kilimo Cha korosho na ufuta lenye ukubwa wa hekari 70.



Pwani Leo
Toleo Maalum la Mwenge wa Uhuru Kazi iendelee...
Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani

# Geraruma asisitiza mahudhurio Kliniki, lishe Bora kwa wajawazito

**Mkuranga Pwani**
**Na.Nasra Mondwe**

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Sahir Geraruma amesisitiza wajawazito kuanza kliniki mapema na kula lishe bora kwa afya ya mama na mtoto na kuwasihi wanyonyeshe watoto ili wawe na virutubisho kutoka kwa mama.

Geraruma alitoa msisitizo huo wakati akizungumza mara baada ya kuzindua mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Msorwa kilichojengwa kwa fedha za tozo ya miamala kwa gharama ya shilingi milioni 250.

Kuhusu ujenzi, Geraruma alizitaka Halmashauri kuzingatia maelekezo ya ujenzi wa miradi ambayo hutolewa na Serikali kulingana na mradi husika na kuhifadhi nyaraka za matumizi ya fedha kwa ajili ya ukaguzi.

Amesema kutokuwa na taarifa za fedha kunatia Shaka na kuonyesha Kuwa kuna Mazingira ya upigaji .

Nae Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga Hadija Nasir ameshukuru wananchi na wadau kwa kushirikiana na Serikali kuinua maendeleo ya wilaya hiyo.

Amesema katika miradi iliyopitiwa na Mwenge, ipo ya fedha za Serikali, kodi ya wananchi ikiwa ni pamoja na Fedha za Tozo na UVIKO 19 zilizofanikisha ujenzi wa miradi mbalimbali ambayo ina tija kwa jamii.

Mwenge wa Uhuru umepokelewa katika wilaya ya Mkuranga ukitokea Kibiti ambapo ukiwa wilayani humo umekagua miradi 14 yenye thamani ya Sh. Bilioni 12.8.

Miradi iliyopitiwa na Mwenge Wilayani Mkuranga ni pamoja na wa ujenzi wa kituo kidogo cha polisi Kijiji cha Mwarusembe, kukagua jitihada za mradi wa mapambano dhidi ya malaria na VVU/UKIMWI, kituo cha afya Kilimahewa na kuweka jiwe la msingi mradi wa maji Mkuranga na tank kubwa la maji Mkwalia wenye thamani ya Bilioni 5.500.




Miradi mingine iliyopitiwa ni kukagua kazi za vijana useremala Mkuranga Mjini, barabara ya lami mita 400 Vikindu-Sangatini, mradi wa madarasa ya Uviko19 Mwandege Sekondari na kuweka jiwe la msingi shule shikizi Mpera.

PwaniLeo
Toleo Maalum la Mwenge wa Uhuru Kazi iendelee...
Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani

## Miradi yenye Thamani ya Shilini Million 967.82 yatembelewa na Mwenge Wa Uhuru Mafia.

**Mfia pwani,**
**Na.Ayubu Simba.**

Mwenge wa Uhuru umetembelea Jumla ya miradi 15 yenye thamani ya sh. milioni 967.821.5 katika wilaya ya Mafia na kupitisha miradi yote.

Kati ya miradi hiyo miradi mitatu imezinduliwa, nane imetembelewa minne imewekwa jiwe la msingi .

Akikabidhi mwenge wa Uhuru Kisarawe mkuu wa wilaya ya Mafia Mhandisi Martin Ntemo, alisema Serikali Kuu imetoa zaidi ya milioni 900,
Halmashauri 19.1 michango ya uhuru milioni 10 na wananchi 2.290 .

Ntemo alishukuru miradi yote imepitishwa na kudai kwamba mafanikio ya Mafia ni ya mkoa hivyo ushirikiano uliopo ndio utakaofikisha maendeleo zaidi kwa mkoa huo kwa kushindanishwa na mikoa mingine.

Kabla ya makabidhiano ya mwenge Mafia na Kisarawe katika viwanja vya ndege ,uwanja wa ndege wa Mwalimu Julius Nyerere , kiongozi wa mbio za mwenge Kitaifa Sahir Geraruma aliwapongeza Mafia kwa usimamizi mzuri wa miradi ya maendeleo kinachotakiwa kifanywe na wilaya zote na mikoa mingine.

Alisema Mafia inapaswa iendelee kujengwa Ni kisiwa kizuri ,licha ya Mazingira Ni magumu Lakini viongozi wanafanya kazi nzuri ,endeleeni na juhudi hizo kuunga mkono Serikali katika suala zima la kusukuma gurudumu la maendeleo.

Vilevile Geraruma aliwataka viongozi wasichoke kukumbusha wananchi ujumbe wa mbio za mwenge mwaka huu ,ikiwemo Kujitokeza katika Zoezi la sensa agost mwaka huu, mapambano dhidi ya malaria,rushwa , utumiaji wa madawa ya kulevya na kupambana na maambukizi mapya ya VVU.

Akipokea mwenge huo kutoka Mafia, Mei 5 mwaka 2022 ,Mkuu wa wilaya ya Kisarawe Nickson Saimon ,alisema Miradi yote Ina thamani ya Bilioni moja , milioni Mia Tisa arobaini ,elfu mia mbili themanini na mbili ,Mia nane tisini na nane na Senti thelathini na moja (1,940,282,898.31).

Nickson alieleza Kati ya fedha hizo Serikali Kuu 717,392,124.76, Halmashauri 10,000,000, Wananchi 705,858,431.76,wahisani 502,032,341.79 na michango ya mwenge 5,000,000.

"Vijiji 21 kati ya 65 wilayani humo ,urefu wa km.192.99 pia mwenge huu utapitia miradi Nane ambapo mradi mmoja utawekewa jiwe la msingi,miradi minne itazinduliwa na miradi mitatu itatembelewa na kukaguliwa "alifafanua Nickson.

Ukiwa Wilayani Kisarawe Mwenge was Uhuru utapitia miradi ya sekta ya Elimu,Afya Maji na Barabara.



# Pwani Leo

Toleo Maalum la Mwenge wa Uhuru *Kazi iendelee...*

**Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani**

**Matukio mbalimbali ya Mapokezi ya Mbio za mwenge Wilayani Mafia Mkoa wa Pwani**













# PwaniLeo

Toleo Maalum la Mwenge wa Uhuru *Kazi iendelee...*

**Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani**


## Geraruma awataka Viongozi kuwa waadillifu kusimamia miradi ya Maendeleo


**Kibaha Mji pwani,**
**Na.Nasra Mondwe.**


Mwenge wa Uhuru umeingia katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha Mkoani Pwani ukitokea Kisarawe na kutembelea miradi 11 yenye thamani ya sh.Bilioni 1.6.

Akipokea mwenge huo kutokea Kisarawe May 6,2022, katika viwanja vya stendi ya zamani Mailmoja, Mkuu wa wilaya ya Kibaha ,Sara Msafiri alisema ,kati ya miradi hiyo mradi mmoja utazinduliwa ,miwili itawekwa jiwe la msingi ,miwili itatembelewa ,sita ujumbe wa mwenge itapokelewa na mmoja ambao Ni wa Kukabidhi vifaa vya ujenzi Shule ya Sekondari Sofu, huku ukikimbizwa kwenye umbali wa Km. 68.7.

Miradi iliyotembelewa na kukaguliwa Ni Pamoja na Mradi wa malaria Kituo cha Afya Mkoani,Ujenzi wa madarasa Shule ya Sekondari Bundikani, na Mapambano dhidi ya rushwa - Shule ya Sekondari Bundikani.

Akiweka jiwe la msingi Mradi wa Kituo cha Afya Pangani, Kiongozi wa mbio za mwenge Kitaifa Sahir Geraruma, alikemea viongozi kuacha kupuuzia mambo kwenye miradi ya maendeleo ili kujiepusha kuchelewesha miradi huku wananchi wakiendelea kutaabika.

Aliendelea kusisitiza uhifadhi wa nyaraka za miradi kwa Ajili ya kumbukumbu za ukaguzi .

Geraruma aliomba baadhi ya viongozi na watendaji waache kufanya kazi kwa mazoea kwa maslahi ya wananchi.

Miradi mingine iliyopitiwa Ni barabara ya lami Picha ya Ndege - Lulanzi, Kutembelea kiwanda cha Mtanga Polytechnic - Sofu, Kupokea taarifa za lishe, VVU, Sensa ya Watu na Makazi - viwanja vya Kwa Mbonde,kata ya Picha ya Ndege,Kutembelea Kikundi cha Vijana cha Republic kilichopo Mwendapole.

Akipokea taarifa ya dawa za kulevya -kata ya Mwendapole, Geraruma aliwaasa vijana kuacha kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya kwani zinamaliza nguvu kazi ya kundi la vijana.

Aliwataka wachapekazi na kujiingiza katika vikundi mbalimbali vya ujasiliamali kujishughulisha kuliko kupoteza muda kuvuta bangi, ama kutumia madawa ya kulevya ambayo yanaathari kwao kiafya .

Geraruma alitoa Rai kwa wale walio tayari kuacha madawa ya kulevya waache na waanze dawa zitakazowasaidia kuacha kwa kuondoa makali ya wingi wa dawa hizo mwilini (methadone).

Mwenge wa Uhuru umepokelewa Mkoani Pwani Mei mosi na sasa upo Halmashauri ya sita wilaya ya Kibaha, ambapo Halmashauri Tisa zitafikiwa kimkoa.

# PwaniLeo

Toleo Maalum la Mwenge wa Uhuru *Kazi iendelee...*

**Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani**


## Miradi yenye Thamani ya Bilon 47.2 yapitiwa na Mwenge Uhuru Bagamoyo.

**Na.Nasra Mondwe.**

Mkuu wa wilaya ya Bagamoyo, Zainab Abdallah ameeleza miradi 25 yenye thamani ya Bilioni 47.2 inapitiwa na Mwenge wa Uhuru .

Akipokea mbio za Mwenge wa Uhuru leo Mei 8,2022, ukitokea wilaya ya Kibaha,katika eneo la Ruvu Darajani alisema wilaya hiyo ina Halmashauri mbili ambapo Halmashauri ya Chalinze itatembelewa miradi 14 iliyogharimu milioni 937.8 na Bagamoyo miradi 11 yenye thamani ya Bilioni 46.3.

Aidha alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia Bilioni 1.6 fedha za Uviko Chalinze na kujenga madarasa na miradi 66 ya shule za Sekondari .

"Tunamuahidi Rais Samia kuwa hatutamuangusha ,katuteua kumsaidia kazi na hapa kwetu Chalinze na Bagamoyo tunapiga kazi ili kuleta maendeleo"alisema Zainab.

Mbunge Wa Jimbo la Chalinze Ridhiwani Kikwete alisema ushauri, mapungufu wanayopatiwa watayafanyia kazi ili baadae miradi iwe Bora kwa maslahi mapana ya wananchi wa Chalinze.

Kiongozi wa mbio za mwenge Kitaifa Sahili Geraruma alihimiza usimamizi makini wa miradi kwani Serikali inatumia fedha nyingi hivyo inatarajia matokeo chanya yenye tija kwa Watanzania.







# PwaniLeo

Toleo Maalum la Mwenge wa Uhuru *Kazi iendelee...*

Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani


## Jakaya awahimiza Tanzania kushirikiana na Serikali Ili kiendeleza Taifa

**Chalinze pwani,**

**Na.Ayubu Simba.**

Rais Mstaafu wa awamu ya Nne,-Jakaya Kikwete amehimiza Watanzania kushirikiana na Serikali pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan ili kuiendeleza nchi yetu.

Aliyasema hayo ,kama mwananchi wa kawaida kwenye mradi wa kikundi cha vijana Msoga , ambao Mwenge wa Uhuru ulipita kuona shughuli za usafirishaji abiria -pikipiki ambao umegharimu milioni 41.8 kati ya fedha hiyo mil.32.6 Ni mkopo wa asilimia 4 ya vijana kutoka Halmashauri na milioni 9.2 Ni fedha ya wanakikundi .

Kikwete alisema Serikali inahitaji mshikamano wa pamoja na kumuunga mkono Rais, Waziri Mkuu na Serikali ili kufikia malengo kimaendeleo na kiuchumi.

"Hii si shughuli yangu ,nimekuja kushiriki Kama mkazi wa Msoga ,Sina maneno mengi ,naomba tu tushirikiane na Serikali kwa maendeleo yetu wenyewe"alisisitiza Kikwete.

Aliomba viongozi na watendaji kufanyia kazi maelekezo yanayotolewa na wakimbiza mwenge Kitaifa.

Nae mke wa Rais wa awamu ya nne mama Salma Kikwete alisema vikundi hivyo vitumie fedha vizuri na dawa ya kukopa ni kulipa.

"Hapa ndio Kwetu Msoga ,mume wangu ndio kwake ,na mwanetu Ni Mbunge wa Jimbo Ridhiwani na tumejiandaa kwani miradi yetu ipo vizuri,tunawakaribisha Sana ,"alisema Salma.

Kwa upande wake kiongozi wa mbio za mwenge wa Uhuru Kitaifa Sahir Geraruma ,alizitaka Halmashauri kuendelea kutenga fedha za vijana , wanawake na wenye ulemavu ili kuimarisha uchumi wa makundi hayo.

Alitoa Rai fedha hizo ziende kwenye makundi hayo Kama Serikali inavyosisitiza kwa manufaa ya vijana ambao wanalia kukosa ajira Lakini wapo wenye moyo wa kujiajiri.

Awali Mkuu wa wilaya ya Bagamoyo alisema mwenge wa Uhuru ukiwa Chalinze utatembelea miradi 14 yenye thamani ya milioni 937.8 .

Miradi iliyopitiwa ni pamoja a kuweka jiwe la msingi ujenzi wa jengo la wodi ya mama na mtoto pamoja na upasuaji kwa fedha ya tozo.

Miradi mingine ni kuzindua mradi wa ukarabati wa barabara Pingo, kufungua vyumba viwili vya Madarasa na ugawaji wa vifaa vya ujenzi vinavyotokana na asilimia 5 ya mchango ya mwenge, kufungua kituo cha afya Sekondari Imperial, mradi wa kisima Kibiki na kuzindua ujenzi wa madarasa manne ya uviko19.





# PwaniLeo

Toleo Maalum la Mwenge wa Uhuru *Kazi iendelee...*

**Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani**


**Matukio mbalimbali ya Mapokezi ya Mbio za mwenge Halmashauri ya Chalinze Mkoa wa Pwani**





















# PwaniLeo

Toleo Maalum la Mwenge wa Uhuru *Kazi iendelee...*

**Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani**


## Mwenge WA Uhuru umeweka jiwe la Msingi bwawa la ufugaji Samaki TANLAPIA exS Ltd katika halmashauri ya Bagamoyo.

**Chalinze pwani,**
**Na.Nasra Mondwe.**

Mwenge wa Uhuru ,umeweka jiwe la msingi mradi mkubwa wa kimkakati wa ujenzi wa mabwawa ya ufugaji samaki TANLAPI exA Ltd,huko Nianjema Halmashauri ya Bagamoyo, Mkoani Pwani ambao umegharimu dollar milioni 19 sawa na sh.Bilioni 44.6 fedha ya kitanzania.

Awali akipokea Mwenge wa Uhuru wa 2022 ,ukitokea Halmashauri ya Chalinze, May 9,2022, katika viwanja vya shule ya msingi Fukayose, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bagamoyo Shauri Selenda alisema, Jumla ya miradi 11 yenye thamani ya Bilioni 46.308.2 katika kata nne imetembelewa.

Nae Mkuu wa wilaya ya Bagamoyo, Zainab Abdallah alieleza miradi 25 yenye thamani ya Bilioni 47.2 imepitiwa na mwenge huo katika Halmashauri mbili za wilaya hiyo.

Alieleza ,wilaya hiyo ina Halmashauri hizo mbili ambapo Halmashauri ya Chalinze itatembelewa miradi 14 iliyogharimu milioni 937.8 na Bagamoyo miradi 11 yenye thamani ya Bilioni 46.3.

Akielezea kuhusu mradi huo wa ufugaji alibainisha ,Ni uwekezaji mkubwa katika Halmashauri ya Bagamoyo, Afrika Mashariki na kati na Ukanda wa Sahara.

Miradi mingine iliyopitiwa ni pamoja na mradi wa upanuzi wa maji kijiji cha Fukayose, kuweka jiwe la msingi ujenzi wa jengo la upasuaji na wodi ya wazazi na barabara kiwango cha Pavement blocks mita 880.
Mwenge wa Uhuru uliingia Mkoani Pwani Mei mosi na kutembelea miradi 111 yenye thamani ya Bilioni 69.2 ,kwenye Halmashauri Tisa ambapo Mei 10 mkoa huu utaukabidhi Mwenge huo Jijini la Dar es salaam





# Pwani Leo

Toleo Maalum la Mwenge wa Uhuru *Kazi iendelee..*

**Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani**

**Matukio mbalimbali ya Makabidhiano ya mwenge wa Uhuru Mkoa Wa  Pwani kwenda  Dar es salaam**

























